

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya utumishi Serikalini inatangaza nafasi ya kazi 111 za Walimu wa Elimu Mjumuisho kwa ajili ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Unguja na Pemba kama ifuatavyo kwa mchanganuo ufuatao:-

MCHANGANUO WA NAFASI ZA WALIMU MJUMUISHO KWA UNGUJA NA PEMBA

UNGUJA				
NO	WILAYA	MSINGI	SEKONDARI	IDADI
1	Kaskazini 'A'	7	0	7
2	Kaskazini 'B'	7	0	7
3	Kati	21	3	24
4	Kusini	5	2	7
5	Magharibi 'A'	4	0	4
6	Magharibi 'B'	4	3	7
7	Mjini	5	2	7
JUMLA UNGUJA		53	10	61
PEMBA				
	ChakeChake	16	8	24
	Micheweni	7	2	9
	Mkoani	6	2	8
	Wete	6	0	6
JUMLA PEMBA		35	12	47

1. Walimu Grade A Daraja la II (ZPSG – 02) Walimu wa Sekondari - Nafasi 10 Unguja na Nafasi 12 Pemba

Sifa za waombaji

1. Awe Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka 46
2. Awe amehitimu Shahada ya Kwanza ya Elimu maalum (Special Education) au Elimu Mjumuisho (Inclusive Education) au Elimu ya mahitaji maalum (Special Needs Education) au amesomea

Nukta Nundu (Braille) au lugha ya alama (Sign Language) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapindizi ya Zanzibar.

**2. Mwalimu Grade B Sanaa Daraja la III (ZPSD – 08) Walimu wa
Skuli za Msingi - Nafasi 53 Unguja na nafasi 35 Pemba
Sifa za waombaji**

1. Awe Mzanzibari mwenye umri usizidi miaka 46
2. Awe amehitimu Stashahada ya Elimu Maalum (Special Education) au Elimu Mjumuisho (Inclusive Education) au Elimu ya mahitaji maalum (Special Needs Education) au amesomea Nukta Nundu (Braille) au lugha ya alama (Sign Language) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar.

Jinsi ya kuomba:

- Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa maombi ya ajira (Zanajira) kupitia anuani ifuatayo:-
<http://portal.zanajira.go.tz> kuanzia tarehe 31 Mei, 2023 hadi tarehe 7 Juni, 2023.
- Mfumo huo pia unapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini www.zanajira.go.tz.
- Maombi yote yatumwe kwa anuani fuatayo:-
KATIBU,
TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,
S.L.P 1587,
ZANZIBAR
- Muombaji anatakiwa kuanisha nafasi ya kazi na Wilaya anayoomba.

Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia email: helpdesk@zanajira.go.tz au simu Nam. 0773 101012.

AHSANTENI.

